# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS - TAMISEMI

DISTRICT COUNCIL
IKUNGI

NAMBA ZA SIMU
MKUU WA SHULE 0766324233
M/MKUU WA SHULE 0764109889
MHASIBU 0759066296
PATRON 062881857

0734020113
SHULE YA SEKONDARI PUMA
S. L. P 429 - SINGIDA

MZAZI/ MLEZI WA MWANAFUNZI ..................................................................

S.L.P .................................

.............................................

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI PUMA KIDATO CHA TANO HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI MKOA WA SINGIDA MWAKA 2022.**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2022 tahasusi ya HKL. Shule ya sekondari Puma ipo umbali wa Kilometa 1 au mita 1000 mashariki mwa mji wa Puma na kuna usafiri wa pikipiki kwaTsh 1000 hadi shule ilipo. Usafiri wa basi kutoka mjini SINGIDA unapatikana katika kituo cha mabasi kilicho karibu na stendi kuu na nauli ni Tshs 2000 kwa wale watakaotoka Manyara Arusha, Tanga, na Moshi. Lakini wale wanaotokea barabara ya Dar Es Salaam kwa Mikoa ya Dodoma, Morogoro, Iringa, Mbeya na Dar Es Salaam watashukia stendi ya Puma mjini kabla ya kufika Singida Mjini. Kwa wale wanaotokea Shinyanga, Kagera, Kigoma, Geita, Mwanza, Simiyu na Mara kupitia Barabara Kuu inayotoka Mwanza kwenda Dar es Salaam watashukia Kituo cha Puma Mjini kilomita 16 baada ya kupita Singida Mjini

Muhula wa masomo utaanza tarehe **13 Juni 2022**. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **13 Juni 2022**. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **30 Juni 2022**.

## MAMBO YA KUZINGATIA.

### 2.1 SARE YA SHULE.

Sare ya shule hii ni kitambaa chenye rangi ya DARK BLUE , na unatakiwa kushona Suruali mbili zenye marinda 2 na shati 2 nyeupe zenye mikono mirefu. Sare ya michezo kwa shule hii ni bukta ya bluu, raba na Tsh 15,000 kwa ajili ya T-shirt. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba, Soksi jozi mbili nyeusi ndefu, Sweta rangi ya kijivu na tai ndefu rangi ya dark bluu yenye mistari myeupe (tai za wanafunzi).



Scanned with CamScanner

2.2 MICHANGO INAYOTAKIWA KULIPWA NA KILA MZAZI NI -;

ADA NA MICHANGO YA SHULE (Viwango vyote ni kwa fedha ya Tshs)

| S/N | AINA YA MCHANGO | MUHULA WA KWANZA | MUHULA WA PILI | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| i) | Ada | 35,000.00 | 35,000.00 | 70,000.00 |
| ii) | Taaluma | 15,000.00 | 15,000.00 | 30,000.00 |
| iii) | Fedha ya tahadhari (haitarejeshwa) | 5,000.00 | ---- | 5,000.00 |
| iv) | Mchango wa mlinzi | 10,000.00 | ---- | 10,000.00 |
| v) | Mchango wa dawati | 15,000.00 | ---- | 15,000.00 |
| vi) | Mchango wa wapishi | 10,000.00 | 10,000.00 | 20,000.00 |
| vii) | Mchango wa ukarabati | 15,000.00 | 15,000.00 | 30,000.00 |
| viii) | Mchango wa kitambulisho na picha | 6,000.00 | ---- | 6,000.00 |
| ix) | Mchango wa nembo ya shule | 2,000.00 | ---- | 2,000.00 |
| JUMLA | | **113,000.00** | **75,000.00** | **188,000.00** |

NB.

- Kama mwanafunzi ana Bima ya Afya (NHIF) aje nayo wakati wa kuripoti ili awe anaitumia katika matibabu na kama hana Bima ya Afya (NHIF) aje na shilingi elfu kumi (Tshs. 10,000.00) na atapewa maelekezo ya namna ya kuipata huduma ya Bima ya Afya (CHF).

Fedha hizo ADA NA MICHANGO MINGINE zilipwe kwenye Akaunti ya shule Na **5086600060** jina la akaunti ni ***PUMA SECONDARY SCHOOL*** katika benki ya **NMB** na mwanafunzi aje na Pay in slip ILIYOANDIKWA JINA LAKE NA MCHANGANUO WAKE. (MICHANGO **ILIPWE YOTE**)

## MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI

- Ream 1 A4 ya karatasi
- Ream 1 ya ruled paper
- Vitabu vya masomo vya Tahasusi
- Godoro lenye upana wa 3 futi 6 na unene nch 2 1/2
- Mashuka pair mbili rangi ya bluu bahari, Blanket l,mto wenye foronya 1 rangi ya blue , chandarua rangi ya blue 1 na taulo 1
- Vyombo vya chakula ni sahani, bakuli, kijiko na kikombe.
- Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko (ndoo 1 atakabidhi, ndoo nyingine kwa ajili ya matumizi yake)

## VIFAA VYA USAFI VILETWE KAMA IFUATAVYO

- wataleta Jembe 1 na softbroom 1

## MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

- Wizi
- Kutohudhuria masomo zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro Kugoma na kuhamasisha mgomo



Scanned with CamScanner

- Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
- Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
- Ulevi au unywaji pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
- Uvutaji wa sigara
- Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa
- Kusababisha mimba
- Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria ya nchi
- Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
- Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkono katika mazingira ya shule
- Kudharau Bendera yaTaifa
- Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu Kuharibu mali ya umma kwa makusudi.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBUNI SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI PUMA

ELISI W. MLUMBA
MKUU WA SHULE

THE HEADMISTRESS
PUMA SECONDARY SCHOOL
SINGIDA



Scanned with CamScanner

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL AUTHORITY AND LOCAL GOVERNMENT**

PUMA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 429 SINGIDA.

A: MEDICAL EXAMINATION FORM for Year ..............................................

4. To be completed by a medical officer in respect of all form I — VI entrants and new school employee.

TO THE MEDICAL DOCTOR ................................. HOSPITAL/ HEALTH CENTRE BOX ................................

Please Examine ................................. Age ............... Whether is fit to pursue studies/work

Test for
Blood (Red and white) ...............................................................................
Stool examination ...................................................................................
Urinal ..........................................................................................
Syphilis ........................................................................................
Eye ............................................................................................
Ear ............................................................................................
Chest ..........................................................................................
Abdomen .......................................................................................

**B: ADDITIONAL INFORMATION:** Physical defects important, infection or family diseases act ................................................................................

C: I certify that the above-mentioned student is fit to pursue studies Medical Doctor's Signature ................................................................................

Name ...................................................................

Designation ............................................................

Station ................................................................



Scanned with CamScanner

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI PUMA S.L.P. 429 SINGIDA**

## FOMU YA KUKUBALI

(Fomu hii pamoja na fomu ya afya na affidavit **virudishwe shuleni siku ajapo mwanafunzi kuripoti**)

MWANAFUNZI AJAZE SEHEMU HII

1. Mimi .......................................... mvulana nimekubali kujiunga kidato Cha ...................... shule ya sekondari Puma tarehe ........................nitafika shuleni bila kuchelewa. Nitatii sheria na nitaishi maisha mazuri na nitakuwa mwanafunzi Mwenye bidii kwenye masomo na kazi za nje. Sitashiriki katika mgomo, fujo na Makosa ya jinai
2. Kama sitatimizâ sheria na kanuni muhimu za shule hii naomba kŭchukuliwa hatua za kinidhamu hii ni pamoja na kufukuzwa shule kwa makosa yasiyovumilika.

MZAZI/MLEZI AJAZE SEHEMU

1. Mimi .......................................................... Nimekubali mtoto wangu (Jina) ..............................................Asome katika shule ya sekondari Puma kuanzia ...................... naahidi kumpatia vitu vyote vinavyotakiwa kufika navyo shuleni kama ilivyotajwa katika barua ya masharti ya kujiunga na shule.

2. Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria zote za shule nakuishi maisha mazuri na kuwa na bidii kwenye masomo na kazi. Nakiri nitalipa michango iliyoainishwa na sitaleta usumbufu kwa mwanangu na kwa uongozi wa shule.

3. Anwani yangu ya kudumu ni ......................................................

Simu. ..................................................................................................

Sahihi ............................................... Tarehe ...................................

Wageni ninaowaidhinisha kumwona mtoto wangu awapo shuleni

i) ................................................ uhusiano wake ..........................
ii) ................................................ uhusiano wake ..........................
iii) ................................................ uhusiano wake ..........................
iv) ................................................ uhusiano wake ..........................



Scanned with CamScanner